



## SHULE YA UPILI YA MANGU

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1

**MWIGO 2022**

INSHA

MUDA: SAA 1¾

### **MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. Wewe ni mtangazaji wa kituo cha habari cha Ukweli. Umetembelewa na mwenyekiti wa kikundi cha watetezi wa haki za wanawake jimboni kuzungumzia namna wanawake walivyotelekezwa katika jamii ya leo. Andika mahojiano kuhusiana na swala hili.
  - Hii ni insha ya mahojiano
  - Insha iwe na anwani / kichwa
  - Huwa na wahusika wawili
  - Maudhui hutokana na maswali na majibu ya washirirki
  - Mhoji ni mtangazaji
  - Mhojiwa ni mwenyekiti wa kikundi cha watetezi wa haki za wanawake
  - Sura ya mahojiano izingatiwe (mtindo wa tamthilia) maswali na majibu
  - Majina mhojiwa na mhoji au vyeo vyao viandikwe upande wa kushoto wa karatasi
  - Asiponzingatia sura ya mahojiano atolewe alama 4.
  - Mwanafunzi ajihusishe kama mhusika. Asipojihusisha aondolewe alama mbili.

### **Baadhi ya hoja**

- ✓ Mtoto msichana kunyimwa elimu katika baadhi ya jamii.
- ✓ Mtoto msichana kukosa mahitaji ya kimsingi kama vile sodo.
- ✓ Ugavi wa raslimali, majukumu na hata mali kumpendelea mwanaume.
- ✓ Viongozi vijijini kama vile wazee wa vijiji na viongozi wa mabaraza tofauti ni wanaume.
- ✓ Uongozi wa makanisa na huduma za kidini kutengewa wanaume kwa misingi kuwa wahubiri na mitume wote walikuwa wanaume.
- ✓ Wanawake kutotengewa thuluthi tatu ya nyadhifa zote katika magatuzi na serikali kuu kama ilivyopendekezwa katika katiba.
- ✓ Idadi kubwa ya wenyekiti wa kamati mbalimbali za bunge la kitaifa na seneti ni wanaume.
- ✓ Katika sekta ya elimu walimu wengi wakuu ni wanaume hata katika shule za wasichana pekee.

2. Unywanji wa pombe haramu una madhara mengi. **Fafanua**

### **Madhara ya unywaji wa pombe haramu.**

- ✓ Maradhi tofauti hasa ya maini
- ✓ Kupofuka
- ✓ Kufilisika – pesa zote hutumika kwa ulevi
- ✓ Kusambaratika kwa ndoa
- ✓ Vifo
- ✓ Uhalifu – wengi hushiriki uhalifu kama wizi ili waweze kujipatia pesa za kununua pombe haramu.
- ✓ Kutamauka – wengi wanakosa nafasi za kazi kwa sababu ni walevi.
- ✓ Kudorora kwa uchumi wa nchi kwa vile vijana hawafanyi kazi
- ✓ Kutelekeza majukumu ya unyumba
- ✓ Huleta migogoro katika familia

3. Methali – Mгаа na upa hali wali mkavu

- ✓ Kisa kionyeshe hali ambapo mhusika au wahusika wanahangaika / wanafanya juhudi za hapa na pale na mwishowe wanza matunda.
- ✓ Ufanisi uonekane kutokana na juhudi za mhusika

**Tanbihi**

- Kisa kionyeshe pande mbili za methali: Kujibidiisha hapa na pale na kule kufanikiwa.

4. Andika insha itakayomalizia kwa maneno yafuatayo;

**...Hapo ndipo iliponibainikia kuwa nilikuwa nikiogelea baharini pekee kinyume na wenzangu wote.**

- Msimulizi ujipate katika hali ambapo yuko kivyake. Kwa mfano amepotoka na baadaye anagundua wenzake hawajapotoka au anafanya bidii peke yake na wengine wanalaza damu.
- Au anaunga au kupinga jambo Fulani pekee na alidhani wako pamoja na wenzake.

**Tanbihi**

- Mtahiniwa atumie nafsi ya kwanza.